**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

# TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA MITIHANI YA 27 YA KITAALUMA YA PSPTB.

**Dodoma 6 September, 2023**

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi **(**PSPTB) inapenda kuwajulisha wadau wake kuwa, mitihani ya 27 ya PSPTB inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **13/11/ hadi tarehe 17/11/2023**.Watahiniwa wote wanahimizwa kufanya usajili kupitia **https://registration.psptb.go.tz** na kuhudhuria madarasa ya mafunzo.

Mitihani hiyo itafanyika katika vitui vya **Dar es salaam, Moshi, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Zanzibar.**Tarehe ya mwisho kujisajili na kulipia mitihani hii ya 27 ya PSPTB **ni tarehe 21/10/2023**.

**WAOMBAJI WENYE SIFA KWA AJILI YA MITIHANI YA NOVEMBA, 2023:**

(1) Wahitimu wote waliomaliza vyuo vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za shahada, stashahada na astashahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia 2023 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi.

(2) Wafanyakazi wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi wasiokuwa na cheti cha juu cha kitaaluma - CPSP.

(3) Wahitimu wenye taaluma nyingine nje ya ununuzi na ugavi kuanzia ngazi za stashahada, shahada au sifa za kitaaluma kutoka Bodi ya taaluma husika.

**NB.** Watahiniwa wanaorudia mtihani zaidi ya ngazi moja wanaruhusiwa kuunganisha ngazi mbili zinazofuatana katika bloc moja kwa masomo kuanzia mawili hadi Sita tu, na kwa kuzingatia ratiba ya mitihani ya 27 ya PSPTB hivyo, wanashauriwa kuangalia ratiba ya mitihani iliyowekwa kwenye tovuti ya Bodi kabla ya kuomba kufanya mitihani hiyo.

Kwa maelekezo au ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu namba **0738441972** au tuma barua pepe kupitia ***barua@psptb.go.tz*** ***or*** ***examinations@psptb.go.tz.***

**Imetolewa na:**

Shamim A. Mdee

**Meneja Masoko na Uhusiano kwa umma**

*Keko Mwanga (Majengo ya Bohari), S.L.P. 5993, Dar es Salaam. Simu: +255 22 2865860 Nukushi: +255 22 2862138. Tovuti: http://www.psptb.go.tz. Barua pepe: info@psptb.go.tz*